Find this and other free resources at https://maktaba.tetea.org

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

MTIHANI WA TAIFA WA DARASA LA NNE - 2014

055

SOMO: SAYANSI

JINA LA MTAHINIWA: _____

JINA LA SHULE : _____

HALMASHAURI: _____

MKOA: _____

MUDA: SAA 1

MAELEKEZO:

1. Karatasi hii ina sehemu nne, A, B, C na D.
2. Jibu maswali yote kama ilivyoelekezwa katika kila sehemu.
3. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizotolewa katika kila swali .
4. Hakikisha umeandika jina lako, jina la shule, halmashauri na mkoa.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

SEHEMU : A

Jibu swali 1 – 10 kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku pembeni.

1. Kuna hatua .....za kunawa mikono.
   A. sita
   B. Saba
   C. tano
   D. nne

2. Nywele chafu huwa ni makazi ya.....
   A. chawa.
   B. inzi.
   C. kunguni.
   D. kupe.

3. Ugonjwa wa hatari zaidi unaosababishwa kwa kufanya ngono zembe.....
   A. kaswende.
   B. ukimwi .
   C. kisonono.
   D. ebola.

4. Sehemu za mwili zinazounganisha nyama na mifupa huitwa.....
   A. ngozi.
   B. viungo.
   C. mifupa.
   D. misuli.

5. Kifaa cha kupima uzito hujulikana kama..... .
   A. themometa.
   B. kapani.
   C. rula.
   D. silinda kipimio.

6. Maji kutoka katika vyanzo vyake huwa katika hali ya.....
   A. kimiminika.
   B. gesi.
   C. barafu.
   D. mvuke.

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org
Scanned with CamScanner

Find this and other free educational resources at https://maktaba.tetea.org

7. Kipi kati ya vitu vifuatavyo hakionekani nyakati za usiku?.
   A. Mwezi.
   B. Nyota.
   C. Jua.
   D. Mawingu.

8. Vifuatavyo ni vyanzo vya mwanga isipokuwa.....
   A. sumaku.
   B. kandili.
   C. mshumaa.
   D. jua.

9. Mchoro huu unaonyesha kifaa kiitwacho .....

   A. mundu.
   B. reki.
   C. kisu.
   D. panga.

10. Binadamu ana aina ngapi za meno?
   A. Tano
   B. Nne
   C. Nane
   D. Tatu

SEHEMU: B

Jibu swali la 11 – 17 kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

11. Kuna hali kuu .....za maada.

12. Huduma ya kwanza hutolewa ili kuokoa..... .

13. Kifaa chochote kinachotumika kurahisisha kazi huitwa.....

14. Mmea hukua mbegu inapoanza.....

15. Jua, umeme na msuguano ni vyanzo vya..... .

16. Ugonjwa wa kwashakoo husababishwa na ukosefu wa.....mwilini.

17. Asilimia .....ya mwili wa binadamu ni maji.

Find this and other free educational resources at: https://maktaba.tetea.org
Scanned with CamScanner

SEHEMU: C

Jibu swali la 18 – 20 kwa kuandika "KWELI" au "SI KWELI"

18. Hali ya mtu kupotewa na fahamu ni kuzirai.....

19. Homa ya matumbo ni ugonjwa unaoenezwa kwa njia ya hewa.....

20. Dainamo ni chanzo kimojawapo cha umeme.....

SEHEMU: D

Jibu swali la 21 – 25 kwa kuoanisha fungu "A" na fungu "B" kwa kuweka herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

NA.	FUNGU: A		FUNGU: B
21	Petali	( )	A. Sauti iliyoakisiwa.
22	Mazingira	( )	B. Wanyama wanaonyonyesha.
23	Ovari	( )	C. Ni sehemu yenye rangi, huvutia wadudu.
24	Mwangwi	( )	D. Hutunza chembe kike.
25	Mamalia	( )	E. Maeneo na vitu vinavyotuzunguka.
		( )	F. Inapokea chavua kutoka kwenye stameni.
			G. Hifadhi ya misitu.
			H. Sauti iliyokwaruzwa.

Find this and other free educational resources at:
https://maktaba.tetea.org
Scanned with CamScanner